

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA THELATHINI NA TISA**

**30 MEI, 2019**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA – TAREHE 30 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka 2017/2018 (*The Annual Report and Audited Accounts of The Arusha International Conference Centre for the Year 2017/2018*).

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **324. MHESHIMIWA GOODLUCK ASAPH MLINGA (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Ulanga ni machache, madogo na machakavu hasa yale ya kulaza Wagonjwa;

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo na ujenzi wa majengo mapya.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**325. MHESHIMIWA RUTH HIYOB MOLLEL (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Migogoro ya Wakulima na Wafugaji imekuwa tatizo sugu katika maeneo mengi nchini pamoja na kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali:-

- (a) Je, Serikali imetenga kiasi gani cha bajeti kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi nchi nzima;
- (b) Kijiji cha Matenzi Kata ya Beta Wilayani Mkuranga kina Wafugaji takribani 10,000. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupima eneo hilo kabla migogoro haijaanza.

**326. MHESHIMIWA ZAINABU MNDOLWA AMIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Wananchi wengi wamejenga makazi yao bila kuzingatia

mipango Miji na matokeo yake kuvunjiwa nyumba zao bila kupata fidia pindi Serikali inapoanza ujenzi unaozingatia mipango Miji:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwapatia Wananchi elimu stahiki ili waepukane na adha hiyo.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**327. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kampuni ya Azam Marine ambayo inafanya biashara ya kusafirisha abiria kwa kutumia boti kwa kupitia baharini, huuza tiketi kwa abiria kwa ajili ya safari lakini abiria anapochelewa safari tiketi hiyo huwa haitumiki na hivyo kusababisha hasara kwa abiria pamoja na usumbufu:-

- (a) Je, Serikali inalijua tatizo hilo;
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo hilo.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **328. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-  
Wizara ya Maji ilikubali kurekebisha Mchoro wa Mradi wa Maji kutoka Mto Ruvuma hadi Mtwara ili Vijiji vingi vya Halmashauri ya Nanyamba vipate maji toka Mto Ruvuma:-

- (a) Je, marekebisho hayo yamefikia hatua gani;
- (b) Je, ni Vijiji vingapi vya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba vitanufaika na mradi huo;
- (c) Je, ni lini mradi huo utanza kutekelezwa.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

### **329. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

- (a) Je, ni lini TRA itakaa na Wafanyabiashara wa Tanzania kusikiliza vilio vyao licha ya kila Mkoa unayo Ofisi ya TRA;

(b) Je, ni sababu gani zinazofanya mizigo inayotoka Zambia, Uganda, Kenya, DRC haipati usumbufu inapoingia Jijini Dar es Salaam katika bandari lakini mizigo kutoka Zanzibar inakuwa kero kubwa inapoingia katika Jiji la Dar es Salaam kupitia Bandarini;

(c) Je, ni lini TRA itaweka Ofisi kila Mkoa kusikiliza kero za Wafanyabiashara ambao wanahisi wanaonewa na vile vile kuwaka Mwanasheria kila Ofisi ili pasiwepo na manung'uniko ya Wafanyabiashara kuonewa.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA**  
**30 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**